

Ufalme wa simu wa sasa

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · January 21, 2016

Mafundisho ya Msingi ya Kanisa Katoliki: Makala za Katoliki · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Ushauri kuhusu mambo mbalimbali Katika Maisha

? Asubuhi saa 12 : 00 mtu anaamka, kabla hata HAJAMUSHUKURU MUNGU, kabla hata hajatoka kitandani, kabla hata hajajifunua shuka,

?ATARIPOTI KWA SIMU KWANZA KABLA YA KURIPOTI KWA YEYOTE, NDIO HAPO UNAONA MTU AKIAMKA KABLA HATA HAJASALI KWA MUNGU ANAAMKIA SIMU KWANZA KUIKAGUA, - Nani alinitafuta?

-Nani alini-text? -WhatsApp nani kanitumia msg? - kwenye magroup kuna mpya gani? - Fb kuna post gani kali? - nani kaweka picha kali leo? Nk. Akimaliza KURIPOTI KWA Simu,

faster faster, anapiga kaombi ka kidesturi, sekunde 20 basi. Biblia ipo hapo kando tu ya kitanda, lkn anaona hana muda wa kuisoma. ?BADALA YA KUANZA SIKU NA BWANA, MTU ANAANZA SIKU NA SIMU. Pamoja na kazi za kuutwa, za mtu huyo, lkn atafanyq juu chini, apate muda wa KURIPOTI kwa SIMU. Lakini mtu huyo huyo, hawez kbsa kupata muda wa kujitenga angalau kwa dk 3 tu, kw kutwa nzima ARIPOTI KWA MUNGU KWA NJIA YA MAOMBI.

Ana muda wa kusoma status kwenye social media kutwa nzima, Lkn hana muda kbsa wa kupitia angalau sura moja tu, ya Biblia kwa siku. Ana bundle la dk, sms, WhatsApp kila siku, lkn hana sadaka ya kumtolea Mungu. Umeme ukikatika kutwa moja tu, akakosa kuwa na simu sababu ya chaji, anajisikia mpwekee, siku anaiona ndefuu, anajiona amepungukiwa saana! Lakini huyo huyo, siku nzima inaisha, na ya pili, ya tatu ,

hajawahi kuwa na muda na Mungu wake hata kidogo, na anaona ni sawa tu. Hata ktk siku ya ibada, yale masaa machache tu ya ibada, ambapo inatakiwa iwe ni mtu na Mungu wake tu, bila kuingiliwa na chochote, ?mtu bado hawezi kukaa bila KURIPOTI kwa simu, ibada inaendelea huku mtu kawasha data, na anasoma na kujibu msg zake km kawaida. ? au kama ana kaustaraabu kidogo, atatoka nje, huko anaenda kukagua msg, kuangalia updates nk.

SIMU UNAYO KUTWA, KUCHWA, KIIILA SIKU, YANI HUKUWEZA KUVUMILIA KUIWEKA PEMBENI KWA MASAA TU? ? Swali nauliza, Mtu wa aina hiyo Mungu wake ni nani? " Usiwe na miungu mingine ila mimi". KUTOKA 20 : 3 Kumuabudu Mungu peke yake, ni kumfanya Mungu awe wa KWANZA MOYONI NA MAWAZONI MWAKO. Kumfanya awe kipaumbele kwenye kiila ulitendalo.

?WENGI WAMEZIFANYA SIMU ZAO, ZICHUKUE NAFASI YA MUNGU KATIKA MIOYO, FIKRA NA MAISHA YAO KWA UJUMLA. ?Wamekuwa tayari kupoteza karibu kiila kitu kwa ajili ya simu -

kupoteza marafiki > hawana muda na marafiki zao, wanajifungia ndani, wakichati. - hawana muda na wazazi wao, hata kama wanaishi nyumba moja. > kijana akifika nyumbani, anapitiliza chumbani, ni yeye na simu, ataonekana muda wa kula tu, tena sometimes

hata mezani anakuwa na simu, pale mezani wako wazazi wake kbsa, ndugu zake nk, lkn hajali uwepo wao, anaendelea na simu tu. - Hawana muda na Mungu > Anahakikisha vyovyote itakavyokuwa, muda wa kuwa na simu unapatikana, HATA KAMA HILO LITAMAANISHA KUUPORA MUDA WA MUNGU (muda wa ibada). Atakosa fedha za kusaidia wahitaji, fedha za zaka na sadaka, lkn fedha ya SIMU, (bundles) , lzm inakuwepo. ?Mtu wa aina hiyo,

anaibudu simu bila kujua. ?KITU CHOCHOTE KINACHOUVUTA MOYO KUTOKA KWA MUNGU, KUKIELEKEA CHENYEWE, KITU HICHO KINAJARIBU KUCHUKUA NAFASI YA MUNGU MOYONI. NB: Sio lengo langu kupinga matumizi ya simu, lkn nilitaka tuwe na kiasi.